# Herufi za KIBANTU



Huruma Joseph

This Book is dedicated to:

**LORD NICHOLOUS MUNUO NG'UNI** (LLB E.A)

PRESIDENT-

**UNION OF ALL BANTU PEOPLES OF AFRICA**

AND

SUPREME DEFENDER OF BANTUISM

IN THE WORLD

Kimechapishwa na:

Brilliant Editions Publishing Ltd;
P. O. Box 3031,
Arusha .
TANZANIA.

Barua pepe: brillianteditions1@gmail.com

© Huruma K. Joseph

Toleo la Kwanza, 2020.

ISBN: 978-9976-502-53-4

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kukitoa kitabu hiki
kwa njia yoyote ile bila indhini ya mwandishi

(Fonts za computer za herufi za kibantu zinapatikana kwa maombi kupitia barua pepe hiyo hapo juu. Utatumiwa link utakapo “download” fonts hizo na ku “install” katika computer yako kisha kuanza kuzitumia katika ku “type”)

# Utangulizi

Tunamwita Bantu (ambayo inamaanisha “ mtu) binadamu wa jamii ya watu wanaoongea kati ya lugha mia sita zinazohusiana zinazoitwa Niger-Congo. Katika Afrika, wanapatikana kutoka magharibi kwenda mashariki, yaani kutoka Gabon hadi Comoros na kutoka kaskazini hadi kusini, yaani kutoka Sudani hadi Namibia na Afrika kusini. Makabila haya hufunika sehemu nzima ya kusini mwa Afrika. Wabantu ni wakulima na ambao pia wamepata uashi wa chuma. Maendeleo haya yamewawezesha kutawanyika sehemu mbombali kwa muda wa takriban miaka elfu nne.

Wataalamu wamekadiria kwamba asili ya wabantu ilikuwa katika maeneo ya Kameruni ya Kusini; kutoka huko wasemaji asilia wa Kibantu katika milenia ya pili Kabla ya Kristo walihamia Kongo hadi Zambia. Waliendelea kuhamahama na kupanuka hadi kufika maeneo yote walipo sasa.

Sehemu kubwa ya maeneo ya wasemaji wa lugha za Kibantu zilikaliwa awali na wasemaji wa lugha za Khoisan. Wataalamu wamekisia kwamba Wabantu walifaulu kuenea kutokana na maarifa yao ya kilimo na hasa matumizi ya chuma katika zana za kilimo na pia silaha.

Leo hii Wabantu wanaunganishwa na umoja unaofahamika kama **The Union of All Bantu Peoples of Afrika** wenye makao makuu yake makuu jijinii Arusha.

Herufi za kibantu ni alama za kubuni zinazoweza kutumika katika mawasiliano ya kimaandishi. Wamishenari wa mwanzo katika pwani ya Afrika ya mashariki waliandika lugha za kibantu kwa kutumia alfabeti za kirumi kwa ajili ya uinjilishaji, baadaye waliendelea kufanya hivyo walipoiandika lugha kiswahili. Swali la kujiuliza kirumi na kibantu ni wapi na wapi?

Hivyo basi kuna haja ya wabantu kutumia herufi zetu wenyewe. Herufi hizi za kibantu ni zao la utamaduni wa wabantu. Kila herufi inawakilisha sehemu ya tunu au dhana mahususi katika utamaduni na mila za wabantu. Herufi zimepitishwa na Umoja wa Wabantu Afrika.

Kila mbantu anahaki ya kujua na kuzitumia herufi za kibantu katika mawasiliano. Kwa kujua herufi za kibantu utaweza kusoma maarifa yaliyoandikwa kwa alfabeti za kibantu. Pia ni fahari iliyoje kuwa na ujuzi wa herufi zetu wenyewe. Mbona Wachina, Wahindi na Warusi wana alfabeti zao wenyewe? Wahabeshi je? ndio wahabesh ambao idadi yao si kubwa kuzidi Wabantu, nao wanaherufi zao zinazofundishwa mashuleni. Ni matumaini yetu kuwa Umoja wa Afrika (AU) utazitangaza herufi hizi n kuwa tunu na kielelezo cha mwafrika.

**Huruma Kilakuno Joseph**
Mwandishi- Arusha, 2020

# AINA ZA HERUFI ZAKIBANTU

Herufi  za Kibantu zimegawanyika katika makundi matano (5) kama inavyofafanuliwa hapa chini. Herufi zinazoonekana katika kila kundi ni kama zilivyo katika mwandiko wa mkono. Hata hivyo mwandiko wa computer,  fonts zinaweza kuwa na vikonyo  au zisiwe na vikonyo (serif or sans serif letterform )



## 1. Herufi za umbo la ngao

Wabantu hujilinda dhidi ya maadui kwa ngao. Maadui hao waweza kuwa binadamu au wanyama. Kundi la herufi za ngao lina memba watano (5).

**Ufafanuzi wa kila herufi**

| Herufi | Jina | matamshi | Herufi mlandano za kirumi |
|---|---|---|---|
|  | nza | \a\ | A |
|  | boda | \b\ | B |
|  | nchili | \ch\ | C |
|  | dra | \d\ | D |
|  | eto | \e\ | E |

# 2. Herufi za umbo la mmea

Kundi hili lina herufi 5. Mojawapo ya shughuli za wabantu ni kilimo. Wabantu hulima nafaka kama mahindi, mtama na ulezi. Pia hulima kunde, karanga na njugu kutegemeana na eneo, jografia  na tabia nchi ya mahali.




**Ufafanuzi wa kila herufi**






| Herufi | Jina | matamshi | Herufi mlandano za kirumi |
|---|---|---|---|
|  | ndafu | \f\ | F |
|  | gigi | \g\ | G |
|  | hala | \h\ | H |
|  | ika | \i\ | I |
|  | Jeki | \j\ | J |

# 3. Herufi za umbo la kibuyu

Kibuyu ni chombo cha asili cha kuhifadhia maji, maziwa na hata unga. Wabantu wamekuwa wakitumia vibuyu tangu enzi na enzi. Herufi za kibantu zenye umbo la kibuyu ni tano.



**Ufafanuzi wa kila herufi**

| Herufi | Jina | matamshi | Herufi mlandano za kirumi |
|---|---|---|---|
|  | kwi | \k\ | K |
|  | lapa | \l\ | L |
|  | mimo | \m\ | M |
|  | ndwele | \n\ | N |
|  | oya | \ ȯ\ | O |

# 4. Herufi za umbo la mundu

Mundu (sickle) ni kifaa kinachotumiwa na wabantu katika shughuli za mavuno. Mazao kama ulezi na mpunga huvunwa kwa kutumia mundu. Kuna herufi 4 za kimundu katika mfumo wa herufi za kibantu.



**Ufafanuzi wa kila herufi**

| Herufi | Jina | matamshi | Herufi mlandano za kirumi |
|---|---|---|---|
|  | pasi | \p\ | P |
|  | rasi | \r\ | R |
|  | sasi | \s\ | S |
|  | tui | \t\ | T |

# 5. Herufi za shape ya kibantu

Wakati ulimwengu wa kimagharibi huchukulia uwembamba wa mwanamke kama mrembo, wabantu wao ni tofauti. Kwao urembo wa mwanamke ni kujazia. Herufi tano za mwisho zimeundwa kwa kufungusha nyuma kama kielelezo cha urembo wa kibantu (massive backside).



**Ufafanuzi wa kila herufi**

| Herufi | Jina | matamshi | Herufi mlandano za kirumi |
|---|---|---|---|
|  | uzi | \ ü \ | U |
|  | vumo | \v\ | V |
|  | wowo | \w\ | W |
|  | yaya | \y\ | Y |
|  | zeze | \z\ | Z |

# Uandishi wa maneno

Katika kuandika maneno, herufi za kibantu hufuata utaratibu maalumu kama wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili,  ambao ni:

A. Herufi kama konsonanti na irabu ambapo huweza kuunda silabi.
Mfano    ba    ma    ka    la



B. Konsonanti, konsonanti na irabu.
Mfano:    kwa    gha    mwa



C. Konsonanti, konsonanti, konsonati na irabu.
Mfano:    mbwa    ngwe



**Soma kifungu kifuatacho cha maneno:**

Maandishi ya kibantu yameficha maarifa muhimu ambayo mjuzi wa alfabeti za kibantu pekee ndiye anayeweza kuyajua. Hivyo ni muhimu sana kwa mbantu au mtu yeyote kuzijua herufi hizo.

**Kwa herufi za kibantu, kifungu hicho kitaandikwa hivi:**

